



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
MKOA WA NJOMBE**

Novemba 24, 2022

TAARIFA KWA UMMA

Mkuu wa Mkoa wa Njombe Mhe. Anthony Mtaka leo Novemba 24, 2022 ameongoza kikao cha Bodi ya Barabara kilichofanyika katika ukumbi wa Halmashauri ya Mji Njombe.

Pamoja na mambo mengine zimewasilishwa taarifa ya Matengenezo ya Barabara kutoka TANROADS na TARURA, Taarifa ya Utekelezaji kuanzia Julai hadi Juni 2022 kwa mwaka wa fedha 2021/2022, Taarifa ya Utekelezaji wa Matengenezo na Ukarabati kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

Katika hatua nyingine Mkuu wa Mkoa wa Njombe Mhe. Anthony Mtaka kesho Novemba 25, 2022 ataongoza kikao cha Kamati ya Ushauri ya Mkoa wa Njombe kitakachofanyika katika ukumbi wa Halmashauri ya Mji Njombe kuanzia saa mbili kamili asubuhi.

Kikao hicho kitahudhuriwa na Viongozi mbalimbali akiwemo Katibu Tawala Mkoa wa Njombe, Wakuu wa Wilaya, Makatibu tawala wa Wilaya, Wenyeviti wa Halmashauri, Wakurugenzi Watendaji wa Halmashauri.

Katika kikao hicho zitawasilishwa taarifa ya matokeo ya sensa ya watu na makazi ya mwaka 2022, taarifa ya maendeleo ya sekta ya afya, elimu na madini.

Chrispin B. Kalinga
Kaimu Afisa Habari na Mawasiliano Serikalini
Mkoa wa Njombe.